Jikinge, jilinde, Chukua Tahadhari

Januari

# TIRA Updates 2026

Kwa Soko Salama la Bima

Toleo No.14 | Jarida la Mtandaoni | www.tira.go.tz



HALIUZWI

## Bima kwa Jamii yenye Afya, Usawa na Ustawi Endelevu

Wasiliana nasi coi@tira.go.tz | Au tupigie +255 222 132 537 | YT, IG, FB, LinkedIn: //@tira_tz

# NENO KUTOKA KWA KAMISHNA WA BIMA

## UHALALI WA UFANYAJI BIASHARA YA BIMA TANZANIA

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 3 cha Kanuni za Bima za mwaka 2009, watoa huduma za bima wote ikiwemo kampuni za bima wanatakiwa kuhuisha leseni ya biashara kabla au ifakapo tarehe 31 Desemba kila mwaka ili kuwapa uhalali wa kuendelea kufanya biashara ya bima nchini. Hata hivyo, kutokana na maombi kutoka kwa watoa huduma za bima, TIRA iliongeza muda wa kuhuisha leseni hadi tarehe 31 Januari, 2026 ili kutoa fursa kwa watoa huduma wote kuhuisha leseni zao kwa mujibu wa Sheria ya Bima Sura ya 394.

Licha ya TIRA kutoa fursa hiyo, imebainika kuwa baadhi ya watoa huduma za bima wameshindwa kuhuisha leseni zao kwa mujibu wa Sheria. Hivyo, Umma unafahamishwa kuwa, watoa huduma wote zikiwemo kampuni za bima ambazo hazijahuisha leseni zao, hawana uhalali wa kufanya shughuli za bima ikiwemo;

i) Kuandikisha au kuchukua vihatarishi vipya vya bima;
ii) Kutoa au kuhuisha hati za bima; (insurance policies renewals); na
iii) Kutangaza au kufanya matangazo ya biashara ya bima.

Kampuni au mtoa huduma yeyote wa bima atakayebainika kuendelea kufanya biashara au shughuli za bima bila kuwa na leseni halali kutoka TIRA, atakuwa amekiuka Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo hivyo atachukuliwa hatua stahiki ikiwemo kutozwa adhabu, kusimamishwa kufanya biashara, au kuchukuliwa hatua nyingine kwa mujibu wa Sheria ya Bima Sura ya 394.

Umma unahimizwa kuhakiki uhalali wa leseni za kampuni za bima au mtoa huduma za bima kabla ya kufanya muamala wowote wa biashara ya bima kwa kuangalia orodha ya kampuni za bima au watoa huduma za bima wenye leseni halali kupitia tovuti ya TIRA ambayo ni www.tira.go.tz au kuhakiki taarifa za kampuni au watoa huduma za bima kupitia TIRAMIS App kwa kuingiza Na. ya usajili iliyotolewa na TIRA au kufika Ofisi ya TIRA iliyokaribu.

Aidha watoa huduma za bima wanahimizwa kuhuisha leseni zao ili kuendelea kuwa na uhalali wa kufanya biashara ya bima na endapo kuna mtoa huduma yeyote mwenye changamoto awasiliane na TIRA.

Taarifa hii kwa Umma imetolewa kwa lengo la kulinda maslahi ya wateja wa bima na kuhakikisha kuwa kuna uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika ufanyaji wa biashara ya bima ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



**Dkt. Baghayo A. Saqware**
**Kamishna wa Bima Tanzania**

# Je unafahamu Majukumu ya TIRA katika Utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote

Kufuatia kutungwa kwa **Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote**, Sura ya 161, mwaka 2023 na kuanza kutumika rasmi tarehe 16 Agosti 2024, Serikali imeweka msingi wa kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za afya bila kikwazo cha kifedha.

Sheria hii inalenga kujenga mfumo shirikishi unaowezesha wananchi wote kupata bima ya afya kupitia michango au michango inayodhaminiwa na Serikali kwa makundi maalum.

Aidha, kutungwa kwa **Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote** ni njia itakayowezesha nchi kufikia lengo Namba 3 katika Malengo ya Maendeleo Endelevu la kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wote linafikiwa ifikapo mwaka 2030.

Utekelezaji wa Sheria hii umekuwa ni sehemu ya Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 na mwaka 2025; na pia ni miongoni mwa Vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 vitakavyowezesha Taifa kufikia Uchumi wa Kati.

Majukumu ya TIRA katika usimamizi wa mfumo wa bima ya afya nchini yameainishwa katika Kifungu cha 7(2) cha **Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote** kama ifuatavyo:

Kwa madhumuni ya kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa mfumo wa bima ya afya kwa wote, Mamlaka itakuwa na wajibu wa;

(a) Kusajili skimu za bima ya afya;
(b) Kuhakikisha bima za afya zinatoa kitita cha mafao ya huduma muhimu kwa mujibu wa Sheria hiyo;
(c) Kuhakikisha huduma za bima zinazotolewa zinaendana na viwango vya michango;
(d) Kutoa miongozo ya malipo kwa watoa huduma;
(e) Kutoa miongozo ya uendeshaji wenye ufanisi na tija katika usimamizi wa skimu za bima ya afya;
(f) Kuhakikisha kuwa skimu ya bima ya afya ina ukwasi na akiba kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa;
(g) Kutunza kanzidata ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyoingia mikataba na skimu za bima ya afya;
(h) Kufanya ukaguzi wa skimu za bima ya afya;
(i) Kuweka miongozo kuhusu usajili wa wanachama katika skimu za bima ya afya;
(j) Kuomba au kuitisha taarifa yoyote itakayoihitaji;
(k) Kufanya tafiti na uvumbuzi kwa lengo la kuendeleza ufanisi na uendelevu wa mfumo wa bima ya afya kwa wote; na
(l) Kutekeleza jukumu lingine lolote kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa Sheria hiyo.

TIRA imeendelea kuratibu, kusimamia, na kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Woite ili kuhakikisha malengo ya Serikali yanatimia.

# Yaliyomo

01



**Jarida Hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma**

**Mhariri**
Hadija Maulid

**Waandishi**
Tabia Mchakama
Anna Massao
Alfred Mlonganile

**Msanifu**
Abubakari W. Kafumba

01 TIRA Yapanda Miti 200 Kuunga Mkono Kampeni ya Tanazania ya Kijani

03 Bima za Wageni kutoka Nje Zisimamiwe Kikamilifu - Waziri wa Mambo ya Nje

04 Bima ya Afya kwa Wote: Kwa Huduma za Afya Bora, Endelevu na za Uhakika kwa Watanzania

06 Kampuni za Bima Zashiriki Wiki ya Huduma za Fedha, Zahimizwa Kuimarisha Utoaji Elimu

09 Zoezi la Ukaguzi wa Bima za Vyombo vya Moto Lashika Kasi Shinyanga na Kahama

10 Elimu ya Bima ya Afya kwa Wote Yatolewa kwa Viongozi wa Wilaya ya Ilemela

12 TIRA Kanda ya Ziwa Yafanya Kikao Kazi na Mameneja wa Kampuni za Bima

13 TIRA Yaipongeza SanlamAllianz kwa Kufungua Tawi Zanzibar

12 Matukio kwenye Vibango

TIRA Updates ni jarida la mtandaoni linaloandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, likilenga kutoa taarifa muhimu, kuelimisha, na kuhamasisha umma kuhusu sekta ya bima nchini. Jarida hili limeandaliwa ili kufikia wadau mbalimbali wa sekta, wakiwemo mawakala wa bima, kampuni za bima, watoa huduma na watumiaji wa bima.

Jarida la TIRA Updates lina taarifa za matukio mbalimbali, ikijumuisha uzinduzi wa miradi mipya, semina, warsha za mafunzo, na mikutano muhimu inayofanyika ndani ya sekta ya bima.

Mbali na taarifa za matukio, TIRAUpdates lina makala maalumu zinazolenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima.

Aidha, toleo hili litaangazia matukio, habari na taarifa muhimu za mwezi Juni 2026.




Scan
Kusoma Kidijiti

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe
**info@tira.go.tz**

Au
Piga simu bure **+255 222 132 537**

Tovuti yetu
**www.tira.go.tz**

# TIRA Yapanda Miti 200 Kuunga Mkono Kampeni ya Tanazania ya Kijani



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) tarehe 27 Januari 2026, imepanda miti 200 kuzunguka eneo la Ofisi ya Makao Makuu jengo laTIRA BIMA House iliyopo Njedengwa Dodoma, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono Kampeni ya Kijani ya kitaifa pamoja na kuadhimisha siku ya kuzaliwa ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Zoezi hilo limeongozwa na Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware, akiambatana na Wakurugenzi, Menejimenti ya TIRA na baadhi ya watumishi. Ushiriki huo umeonesha dhamira ya TIRA katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kulinda mazingira na kuhimiza matumizi endelevu ya rasilimali za asili kwa maendeleo ya taifa.

Akizungumza wakati wa tukio hilo, Dkt. Saqware alisema kuwa upandaji wa miti ni sehemu ya mchango wa TIRA katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, kuboresha mazingira ya kazi na makazi, pamoja na kuhakikisha urithi wa mazingira bora kwa vizazi vijavyo. Pia amesisitiza Taasisi za umma zina wajibu wa kuwa mfano katika kutekeleza ajenda ya uhifadhi wa mazingira kwa vitendo.

Aidha, Dkt. Saqware amebainisha kuwa kuadhimisha siku ya kuzaliwa ya Mheshimiwa Rais kwa vitendo kama upandaji miti ni ishara ya kuunga mkono maono yake ya uongozi unaojali mazingira, ustawi wa jamii na maendeleo jumuishi.

Katika hatua nyingine, Kamishna wa Bima amesisitiza umuhimu wa utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote (UHI), akiwahimiza Watanzania na viongozi katika ngazi zote

kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha wananchi kujiunga na mfumo huo. Alifafanua kuwa Bima ya Afya kwa Wote inalenga kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora, endelevu na za uhakika za afya bila vikwazo vya kifedha, jambo litakalosaidia kuongeza tija ya wananchi na kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Dkt. Saqware aliongeza kuwa TIRA itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa bima kwa ujumla, hususan bima ya afya.

Zoezi hilo la upandaji miti limefanyika katika hali ya mshikamano, uzalendo na uwajibikaji, likionesha dhamira ya TIRA katika kuunga mkono juhudi za Serikali na kuenzi maono ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Tanzania ya kijani, yenye afya njema na maendeleo endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.












# Bima za Wageni kutoka Nje Zisimamiwe Kikamilifu - Waziri wa Mambo ya Nje




Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Balozi Mahmoud Thabiti Kombo, tarehe 04 Januari 2026, ametembelea banda la Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Zanzibar (ZITF), ambapo ametoa maelekezo muhimu kuhusu masuala ya bima kwa wageni wanaotembelea nchini.

Katika ziara hiyo, Waziri Kombo alipata fursa ya kuelezwa kuhusu majukumu ya TIRA katika kusimamia na kuendeleza sekta ya bima, hususan katika kuhakikisha ulinzi wa maslahi ya wageni kutoka nje wanaoingia Tanzania kwa madhumuni ya utalii, biashara na shughuli nyingine.

Waziri Kombo amesisitiza umuhimu wa kuwepo kwa mifumo madhubuti ya bima kwa wageni ili kulinda usalama wao, kuongeza imani ya wawekezaji na watalii, pamoja na kuimarisha taswira ya Tanzania kimataifa kama nchi salama na yenye mazingira rafiki ya uwekezaji na utalii.

Aidha, ameelekeza wadau wa bima kushirikiana kwa karibu na taasisi za Serikali zinazohusika na masuala ya uhamiaji, utalii na afya hasa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili kuhakikisha bidhaa za bima kwa wageni zinaeleweka, zinapatikana kwa urahisi na zinakidhi mahitaji halisi ya soko la kimataifa.

Kwa upande wake, Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Kanda ya Unguja, Ndg. Kurenje Mbura amemuhakikishia Waziri Kombo kuwa TIRA itaendelea kusimamia sekta ya bima kwa weledi na kushirikiana na wadau wote ili kuboresha huduma za bima kwa wageni wa nje na mizigo inayoagizwa kutoka nje jambo litakalosaidia kukuza sekta ya utalii, biashara na uchumi wa taifa kwa ujumla.

TIRA ilishiriki Maonesho hayo kuelekea Maadhimisho ya miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar, na yalianza tarehe 29/12/2025 na kumalizika tarehe 16/01/2026 katika Viwanja vya Nyamanzi Dimani Zanzibar.

# Bima ya Afya kwa Wote: Kwa Huduma za Afya Bora, Endelevu na za Uhakika kwa Watanzania




Serikali imetangaza kuanza rasmi kwa awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote inayolenga kuwahudumia wananchi wasio na uwezo kuanzia tarehe 26 Januari 2026.

Katika awamu hii ya kwanza Kaya zitasajiliwa kwa kiasi cha shilingi 150,000/= kwa mwaka (kaya isiyozidi watu 6). Wananchi wasio na uwezo, wakiwemo wazee, watoto, wajawazito na watu wenye ulemavu, wataendelea kugharamiwa na Serikali.

Akizungumza tarehe 23 Januari 2026 jijini Dodoma katika Kikao Kazi cha Kujadili Utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote kilichowakutanisha viongozi na watendaji wa ngazi za mikoa, wilaya na serikali za mitaa, Waziri wa Afya, Mhe. Mohamed Mchengerwa, amesema mpango huo unalenga kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma bora, endelevu na za uhakika za afya kupitia skimu za bima ya afya zilizosajiliwa.

Ameeleza kuwa, gharama hiyo itamhusisha mwanachama mkuu, mwenza wake pamoja na wategemezi wanne huku utoaji wa huduma ukizingatia utaratibu wa rufaa katika vituo vya afya vilivyoingia mikataba na skimu za bima ya afya.

Akiwasilisha mada katika kikao hicho, Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo A. Saqware, ameeleza majukumu TIRA katika kusimamia utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote akibainisha kuwa, Mamlaka imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kimkakati ili kuhakikisha

Sheria hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Aidha, mefafanua kuwa miongoni mwa vipaumbele vya TIRA ni utoaji wa elimu kwa umma kwa lengo la kujenga uelewa mpana kwa Watanzania na kuhakikisha hakuna mwananchi anayeachwa nyuma katika utekelezaji wa mpango huo.

Dkt. Saqware ameongeza kuwa TIRA itaendelea kuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kuwekeza katika mifumo ya kisasa ya usimamizi wa bima, sambamba na maelekezo ya Serikali kama alivyoeleza Waziri wa Afya, Mhe. Mohamed Mchengerwa.

Pamoja na hayo, amesema lengo kuu ni kuhakikisha wateja na wanufaika wa bima wanapata huduma bora kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

TIRA imeandaa muongozo maalum unaoainisha utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko yanayohusiana na utoaji wa huduma za Bima ya Afya kwa Wote, kwa lengo la kutatua changamoto zitakazojitokeza na kuimarisha ulinzi wa wanachama wa bima.

Wakati huo, Serikali imezitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa, viongozi na watendaji katika ngazi zote kushirikiana kikamilifu katika kuhakikisha elimu sahihi kuhusu Bima ya Afya kwa Wote inawafikia wananchi kwa wakati, ili kufanikisha azma ya Serikali ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa Watanzania wote.







# Kampuni za Bima Zashiriki Wiki ya Huduma za Fedha, Zahimizwa Kuimarisha Utoaji Elimu




TIRA pamoja na wadau wa Bima wameshiriki katika Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yaliyofanyika viwanja vya Usagara Tanga kuanzia tarehe 16 -24 Januari 2026.

Akiongea na wadau katika maadhimisho hayo Naibu Kamishna, Bi. Khadija Said amezipongeza kampuni za bima kwa ushiriki wao ambao umekua mchango mkubwa na muhimu katika kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu huduma za bima na ulinzi wa kifedha.

Wakati akitembelea mabanda ya kampuni hizo, Bi. Khadija amesisitiza umuhimu wa kuendelea kutoa elimu ya bima kwa makundi yote ya jamii, hususan vijana na wafanyabiashara wadogo, ili waweze kufanya maamuzi sahihi ya kifedha na kujikinga dhidi ya vihatarishi mbalimbali huku akisisitiza zaidi juu ya uelimishaji kuhusu bima ya afya kwa wote.

Kampuni zilizoshiriki ni pamoja NIC, ZIC, Bumaco, Meticulous Gen. Insurance, Sanlam Allianz,MO Assurance, Britam Insurance, Newtan Insurance na kampuni ya bima mtawanyo ya Grand Re.


#sisindiyobima
MAADHIMISHO YA WIKI YA
HUDUMA ZA FEDHA KITAIFA
"Elimu ya Fedha, msingi wa maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi"
MANDATORY
INBOUND TRAVEL
INSURANCE
NIC
SISI NDIYO BIMA
NIC
SISI NDIYO BIMA


GRAND RE
GRAND RE
GRAND RE
GRAND RE
GRAND RE


Britam
With you every step of the way


DIRA
MAJUKUMU YA MSULUHISHI WA MIGOGORO YA BIMA
TUNU ZA MSULUHISHI WA MIGOGORO YA BIMA
DHIMA
MAWASILIANO
JENGO LA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
14 - MTAA WA JAMHURI
GOROFA YA CHINI
S. L. P. 2893
11470 DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu: +255 22 2111117
Nukushi: +255 22 2111094
Simu Bure: 0800111122
www.tio.go.tz
THE TANZANIA INSURANCE OMBUDSMAN
TIO
MSULUHISHI WA MIGOGORO YA BIMA

# Zoezi la Ukaguzi wa Bima za Vyombo vya Moto Lashika Kasi Shinyanga na Kahama




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) Kanda ya Magharibi imeratibu na kusimamia zoezi la ukaguzi wa bima za vyombo vya moto katika mikoa ya Shinyanga na Kahama.

Kwa mkoa wa Shinyanga zoezi hilo limefanyika Januari 5 – 6, 2026 na kwa mkoa wa Kahama limefanyika Januari 7 – 9, 2026; ikiwa ni sehemu ya juhudi za TIRA kuhakikisha wamiliki wa vyombo hivyo wanazingatia matakwa ya kisheria ya kuwa na bima halali.

Katika zoezi hilo Mkuu wa Usalama Barabarani Wilaya ya Shinyanga, ACP Zainab Mangala ameeleza umuhimu wa kuwa na Bima kwa vyombo vya Moto nakuongeza  kuwa bima ni jambo la lazima na ni msaada mkubwa yanapotokea majanga hivyo, kuwataka watumiaji wa vyombo vya moto kuhakikisha wanakata bima.

Kwa upande mwingine, Meneja wa TIRA Kanda ya Magharibi Bi. Awanje Matenda amesisitiza kuwa wamiliki wa vyombo vya moto wanatakiwa kukata na kutumia bima halali kutoka kwa kampuni zilizosajiliwa na pia amewarai wasafiri wote kuhakiki chombo cha moto kutumia mfumo wa TIRAMIS kabla ya safari.

Ameongeza kuwa abiria yeyote anaweza kufanya utambuzi wa chombo cha moto kilochokatiwa bima kupitia simu janja.

# Elimu ya Bima ya Afya kwa Wote Yatolewa kwa Viongozi wa Wilaya ya Ilemela



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia Kanda ya Ziwa imetoa elimu kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa viongozi wa Wilaya ya Ilemela Januari 28, 2026 jijini Mwanza, ikiwa ni sehemu ya jitihada za serikali kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma za afya kwa usawa na kwa gharama nafuu.

Elimu hiyo imelenga kuwawezesha viongozi hao kuelewa wajibu wao katika kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo ngazi ya Serikali za mitaa na kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika mfumo wa bima ya afya kwa wote.

Walioshiriki ni pamoja na Kamati ya Usalama ya Wilaya, Mbunge, Madiwani, Watendaji wa kata, mitaa na vijiji, Wenyeviti wa mitaa na vijiji wote wa wilaya ya Ilemela.

Kwa upande wake, Meneja wa TIRA Kanda ya Ziwa, Bw. Oyuke Phostine, amesema TIRA ipo tayari kusimamia utekelezaji wa Sheria hiyo pamoja na kanuni zake katika maeneo yote yaliyo chini ya usimamizi na udhibiti wa TIRA. Ameeleza kuwa TIRA itahakikisha skimu zote za bima ya afya zinafuata sheria, misingi ya haki kwa wanachama na viwango vilivyowekwa ili kulinda maslahi ya wananchi.

Bw. Oyuke ameongeza kuwa TIRA itaendelea na jukumu la kutunza na kuhuisha kanzidata ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya vilivyoidhinishwa, ili kuhakikisha vituo hivyo vinatoa huduma bora, salama na zenye viwango vinavyokubalika.

Aidha, TIRA itaendelea na ukukaguzi wa mara kwa mara wa Skimu za Bima ya Afya ili kuhakikisha zinazingatia matakwa ya sheria na kutoa huduma stahiki kwa wanachama wake kwa lengo la kufanikisha azma ya taifa ya kufikia bima ya afya kwa wote.





# TIRA Kanda ya Ziwa Yafanya Kikao Kazi na Mameneja wa Kampuni za Bima



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanania (TIRA) Kanda ya Ziwa imefanya kikao kazi na Mameneja wa Kampuni za Bima zinazofanya shughuli zake katika kanda hiyo, kwa lengo la kuweka mikakati madhubuti ya kuwafikia wananchi wengi na kuongeza mchango wa sekta ya bima katika pato ghafi la kanda ya Ziwa.

Kaimu Meneja TIRA Kanda ya Ziwa, Bw. Oyuke Phostine, amesisitiza umuhimu wa ushirikiano wa karibu kati ya TIRA na Kampuni za Bima ili kupanua wigo wa huduma.

"Bado kuna idadi kubwa ya wananchi katika kanda ya ziwa ambao hawajafikiwa na huduma za bima, hivyo kunahitajika mikakati ya pamoja ya elimu kwa umma, ubunifu wa bidhaa na matumizi ya teknolojia rahisi ili kuwafikia wananchi wa kada zote" alisisitiza Bw. Oyuke.

Aidha, kikao hicho kimejadili mikakati ya kuongeza pato ghafi la bima katika kanda ya Ziwa kwa kuimarisha mauzo ya bidhaa za bima zinazokidhi mahitaji halisi ya wananchi, hususan katika sekta za afya, kilimo, madini, ufugaji, uvuvi, biashara ndogo ndogo na usafirishaji.

Bw. Oyuke amewahimiza Mameneja wa Kampuni za Bima kuhakikisha wanazingatia viwango vya kitaaluma, maadili ya kazi na ufanisi katika kuhudumia wateja, ili kujenga imani ya wananchi kwa sekta ya bima.

Kikao hicho kimehitimishwa kwa makubaliano ya kuendelea kufanya usajili wa mawakala na mbinu mpya za usambazaji wa bima ili kutekeleza kwa urahisi mikakati iliyopangwa na kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa manufaa ya wananchi na ukuaji wa sekta ya bima katika Kanda ya Ziwa.

# TIRA Yaipongeza SanlamAllianz kwa Kufungua Tawi Zanzibar




Bi. Khadija Said, Naibu Kamishna, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), ameipongeza kampuni ya bima ya SanlamAllianz kwa kufungua rasmi tawi lake Zanzibar, akieleza kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za bima kwa wananchi visiwani humo.

Akizungumza katika hafla ya kuikaribisha rasmi kampuni hiyo ameongeza kuwa uwepo wa kampuni hiyo Zanzibar utaongeza ushindani chanya katika sekta ya bima, kuimarisha utoaji wa huduma bora pamoja na kuongeza uelewa na matumizi ya bima miongoni mwa wananchi na wadau mbalimbali wa kiuchumi.

Hafla hiyo maalum pia ililenga kutambua mchango wa mawakala katika kukuza sekta ya bima, ambapo TIRA imesisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya wadau wa bima kuhakikisha huduma zinawafikia Watanzania wengi zaidi.


EXIT


Sanlam | Allianz
Sanlam Allianz
KARIBU
ZANZIBAR
Life Insurance . General Insurance . Investment

# MATUKIO KATIKA VIBANGO




















# TIRA Updates 2026

HEADQUATERS
TIRA BIMA HOUSE, Njedengwa,
P.O BOX. 2987, Dodoma, Tanzania.

Phone: +255 (026) 232 1180
Fax: +255 (026) 232 1180
E-mail: coi@tira.go.tz
Website: www.tira.go.tz

@tira_tz